OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

HOTUBA YA BW. SAMWEL MARCO MANENO, NAIBU MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI NA MAKAMU MWENYEKITI WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI AKIMKARIBISHA MHE. HAMZA SAID JOHARI MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI NA MWENYEKITI WA BARAZA LA WAFANYAKAZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

UKUMBI WA MIKUTANO WA LUSH GARDEN HOTEL - ARUSHA

27 APRILI, 2026

- **Mhe. Hamza Saidi Johari, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Bi. Beatrice Jeremiah Nzobonaliba, Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,**
- **Bi. Rashid Shabani Kigaru, Mwenyekiti wa TUGHE, Tawi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Mwakilishi wa Vyama vya Wafanyakazi,**
- **Mwakilishi wa Baraza Kuu la Wafanyakazi Serikalini;**
- **Wajumbe wote wa Baraza la Wafanyakazi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;**
- **Waandishi wa Habari;**
- **Wageni Waalikwa;**
- **Mabibi na Mabwana;**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA …..
KAZI NA UTU.....
OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI …....

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha wote kukutana hapa siku ya leo katika kikao hiki muhimu cha Baraza la Wafanyakazi kinachojikita katika kujadili Mipango na Bajeti ya Ofisi ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali kwa mwaka wa fedha 2026/027.

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Katika kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa katika Ibara ya 59 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268, Sheria za kazi na Sheria nyingine za nchi ikiwemo Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama ilivyo kwa taasisi nyingine za umma inapaswa kushirikisha watumishi wake katika kufanya tathmini ya utendaji kazi wake kwa kuzingatia malengo yaliyopangwa, utekelezaji, kujadili changamoto zilizopo na kuweka mikakati ya kuzitafutia ufumbuzi. Kwa muktadha huo, katika Kikao hiki cha leo, pamoja na masuala mengine yatakayojadiliwa, kutakuwa na Ajenda Kuu Mbili. **Ajenda ya kwanza ni kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2025 hadi Machi 2026 na Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2026/2027.**

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2025 hadi Machi 2026, Ofisi ilipokea jumla ya kiasi cha Shilingi **27,519,338,753.06** sawa na asilimia **67** ya bajeti iliyoidhinishwa ya Shilingi **40,941,954,000.00** kwa mwaka 2025/2026. Bajeti hiyo iliyopokelewa inajumuisha **Shilingi 24,108,257,950.06** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo,**Shilingi 3,231,734,491.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na Shilingi **179,346,312.00** kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Arusha. Mchanganuo zaidi wa matumizi ya fedha hizi utawasilishwa na Mkurugenzi wa Mipango katika kikao hiki kama ajenda zilivyoainishwa. Naomba nitumie nafasi hii kuwaeleza kwa kifupi baadhi ya mafanikio yaliyopatikana wakati wa

utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kipindi cha mwezi Julai, 2025 hadi Machi, 2026.

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai hadi Machi, 2026 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kuongeza idadi ya watumishi wa kada mbalimbali kwa utaratibu wa ajira mpya na uhamisho ambapo watumishi **15** wapya waliajiriwa, watumishi **21** wamehamia kutoka taasisi mbalimbali za Serikali, watumishi **14** walipandishwa vyeo, watumishi **5** walifanyiwa recategorization na watumishi **5** walithibitishwa kazini. Hivyo, hadi kufikia Machi, 2026 Ofisi ina jumla ya watumishi **210.**

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2025 hadi Machi 2026, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanikiwa kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika fani mbalimbali kwa watumishi wake na Wanasheria wengine kutoka Taasisi nyingine za Umma. Aidha, Ofisi iliwajengea uwezo watumishi kupitia mafunzo, ambapo watumishi **17** wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu (15 mafunzo ndani ya nchi na 2 mafunzo nje ya nchi), Watumishi **192** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi (**117** mafunzo ndani ya nchi na **75** mafunzo nje ya nchi) na Watumishi 42 walipatiwa mafunzo elekezi.

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Mafunzo mengine yalitolewa kwa Watumishi **138** kuhusu UKIMWI na Virusi vya UKIMWI, magonjwa ya akili na magonjwa yasiyoambukizwa na upimaji wa hiari. Watumishi hao pia walishiriki katika zoezi la upimaji

wa hiari wa Virusi vya UKIMWI. Watumishi **101** walipata fursa ya kupata mafunzo kuhusu masuala ya Maadili na Mkakati wa Taifa dhidi ya Kupambana na Rushwa.

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Kwa upande wa Utekelezaji wa Upekuzi wa mikataba: kuanzia mwezi Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya Mikataba ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa **2,324** ilifanyiwa upekuzi **kati ya mikataba 2,000 iliyokuwa imepangwa** kufanyiwa upekuzi ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia **16** ya utekelezaji. Kati ya mikataba **2,324** iliyofanyiwa upekuzi, mikataba **443** ilithaminishwa katika sarafu mbalimbali ambapo, Mikataba **354** ilikuwa na Thamani ya **Trilioni 4.74**; mikataba **72** ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani **2, 200,246,254.54** sawa na shilingi **Trilioni 6.4** za Tanzania, Mikataba **13** ilikuwa na thamani ya **Fedha ya Jumuiya ya Ulaya (Euro) 1,114,102,270.38** sawa na **Shilingi Trilioni 3.3 za Tanzania** na **Mikataba minne (4)** ilikuwa na thamani ya fedha ya **Pauni (GBP) 881,138,752.00** sawa na **Shilingi Trilioni 3.04 za Tanzania**. Mikataba iliyofanyiwa upekuzi ilihusisha masuala ya ununuzi wa majenzi, na ukarabati wa majengo, utoaji huduma za jamii kama vile ujenzi wa shule, hospitali na barabara, huduma za kitaalam, ununuzi wa bidhaa**.**

Katika kipindi hicho pia, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanikiwa kufanya upekuzi wa Hati za Makubaliano (Memoranda of Understanding) **396 kati ya 600 iliyokuwa imepangwa ambapo ni sawa na asilimia 66 ya utekelezaji.** Hatua hii imeimarisha diplomasia ya kisheria, kuhakikisha ushirikiano wa kimataifa unaleta manufaa ya kiuchumi na kijamii, na kupunguza vihatarishi vinavyoweza kujitokeza katika utekelezaji wa makubaliano hayo.

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Katika kipindi hicho, jumla ya maombi ya ushauri **1,897** yaliyopokelewa kutoka kwenye Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na wadau wengine. Utekelezaji huo ni sawa na ongezeko la asilimia **26.4** ya shabaha ya maombi **1,500** yaliyotarajiwa kupokelewa na kufanyiwa kazi. Ushauri huu umeongeza uhalali wa maamuzi ya Serikali, kupunguza migogoro, kuimarisha utawala bora, na kusaidia taasisi za umma kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria. Kati ya maombi hayo, maombi **241** yalitoka Serikali Kuu (Wizarani), maombi **366** yalitoka Taasisi za Serikali, maombi **29** yalitoka kwenye Mashirika ya Umma, maombi **72** yalitoka Mamlaka za Serikali, maombi **96** Wakala wa Serikali, maombi **54** yalitoka Mamlaka za Serikali za Mtaa, maombi **66** yalitoka kwenye Makampuni; na maombi **973** yalitoka kwa wananchi wa Tanzania.

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Vilevile, Ofisi ilifanikiwa kuratibu na kufuatilia Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati za Kudumu za Ushauri wa Kisheria za Mikoa na Wilaya kwa kuzindua na kuendesha Kliniki bure za Ushauri wa Kisheria katika Mikoa ya Manyara, Simiyu na Dar es Salaam na Wilaya zake. Kamati hizo zimeanzishwa kwa mujibu wa mwongozo wa Huduma za Ushauri wa Kisheria katika Mikoa na Wilaya (*Regional and District Legal Advisory Services (Practice Notes, 2024)).* Kamati hizi zinalenga kutoa ushauri wa kisheria kwa wananchi, watumishi na viongozi wa Umma kwa ujumla ili kutatua changamoto za kisheria zinazojitokeza katika Mikoa na Wilaya husika.

Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 kupitia kliniki hizi, Ofisi imetoa elimu ya sheria kwa wananchi **5,516** na imeshughulikia migogoro **560** ikiwemo migogoro ya Ardhi, Mirathi, Jinai, Madai, Ajira, Ukatili wa kijinsia, Ndoa na Matunzo ya watoto. Mchanganuo wa migogoro hiyo ni kama ifuatavyo: **275** inahusu Ardhi, **37** inahusu Ndoa, **48** inahusu Jinai, **59** inahusu Madai, **31** inahusu Ajira, **24** inahusu Ukatili wa kijinsia, **54** inahusu Mirathi, **10** inahusu Matunzo ya Watoto na **22** inahusu masuala mtambuka. Migogoro hiyo kwa sehemu kubwa imehitimishwa kikamilifu na wananchi kupata haki zao, na zile zilizokuwa zinahitaji uendelevu wa ufuatiliaji zimekabidhiwa kwenye Kamati za Mkoa na Wilaya kwa ufuatiliaji.

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kuboresha Mazingira ya kufanyia kazi kwa kuunganisha Mfumo wa OAG-MIS na Mifumo ya Kesi **(Case Management Systems)** ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Mahakama ya Tanzania. Vilevile, tumefanikwa kuunganisha mfumo wa OAG-MIS na Nest wa PPRA ambao utasaidia kupokea na kufahamu mikataba yote inayowasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mikataba mingine ambayo kwa mujibu wa Sheria hailazimishwi kuwasilishwa katika Ofisi yetu. Pia, kwa sasa zoezi la kuendelea kuboresha mfumo wa OAG-MIS kwa awamu ya pili linaendelea Mkoani Morogoro na wapo asilimia 71 ya utekelezaji. Sambamba na hilo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kutoa Motisha kwa Watumishi, kutoa huduma ya chakula kwa Watumishi, Kuongeza Huduma za Ziada za Afya kwa Watumishi (NHIF) na kuongeza idadi ya vitendea kazi hususan magari na kompyuta mpakato.

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Kuhusu maboresho katika Muundo wa Ofisi, ambapo tarehe 4 Machi 2026 Mhe. Rais aliidhinisha Muundo Mpya wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambapo muundoi mejumuisha Divisheni mpya ya Majadiliano, Usimamizi wa Mikataba na Utatuzi wa Migogoro, Kitengo cha Utafiti na Mafunzo ya Kisheria, Kitengo cha Masijala ya Sheria na Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathimini. Hivyo, mundo ulioidhinisha umekuwa na Divisheni 4, Vitengo 9 pamoja na Ofisi za Mikoa katika mikao 26 ya Tanzania Bara. Lengo ni kuimarisha utoaji wa huduma za kisheria kwa Serikali, kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mikataba na makubaliano ya kimataifa, na kuboresha uratibu wa masuala ya kisheria katika taasisi za Serikali.

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Naomba kutumia fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuhakikisha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali unatekelezwa ipasavyo. Mafanikio haya ni matokeo ya bidii na ushirikiano tulionao. Hivyo, ni rai yangu kwenu tuendelee na moyo huo wa kufanya kazi kwa bidii.

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Katika kuendelea kuboresha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

a) Kufanya mapitio ya vipaumbele vya bajeti ili kuendana na majukumu mapya kutokana na Muundo mpya;

b) Kuendelea kuomba vibali Serikalini vya kuongezewa watumishi kwa utaratibu wa uhamisho kutoka kwenye taasisi kama OSG, NPS, OCPD, ili kuongeza ufanisi katika maeneo mbalimbali;
c) Kuendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA na miundombinu yake kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kidijitali;
d) Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wote kulingana na Mpango wa Mafunzo wa Taasisi wa mwaka 2023/2024 hadi 2025/2026;
e) Kuendelea kutafuta fedha za Miradi ya Maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi unaoendelea Dodoma, Mwanza, Arusha na maeneo mengine yatayopangwa, ununuzi wa magari na vitendea kazi; na
f) Kuendelea na utaratibu wa kufungua Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mikoa mingine tisa ikiwemo Morogoro, Kigoma, Katavi, Songwe, Ruvuma, Singida, Shinyanga, Mara na Iringa katika mwaka huu wa Fedha, na kumalizia mikoa saba (7) inayobaki katika mwaka wa fedha 2026/027.

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Nikiwa naelekea kuhitimisha hotuba yangu, niwasihi Mawakili wote wa Serikali na Watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali waendelee kuzingatia masuala yote yaliyozungumzwa katika hotuba zilizotolewa katika vikao vya Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali vilivyotangulia. Vilevile, tuendelee kuwa na ushirikiano wa karibu na Serikali, Bunge na Mahakama katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi.

Ndugu Mwenyekiti wa Baraza na Wajumbe wa Baraza,

Baada ya kusema hayo, naomba nikukaribishe ili uweze kutoa hotuba yako na kutufungulia rasmi Kikao hiki cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

KARIBU SANA

Samwel M. Maneno
NAIBU MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI
27 APRILI, 2026